

## HALMASHAURI YA WILAYA MLIMBA



### SHULE YA SEKONDARI NAMWAWALA

S.L.P. 342

IFAKARA

TAREHE .....

MZAZI / MLEZI

WA.....

#### **YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NAMWAWALA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021**

Nimefurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Namwawala mwaka 2021. Elewa kuwa nafasi hii ni ya kipekee sana kwake, hivyo hana budi kuitumia vizuri ili siku za usoni ilete manufaa kwake na taifa kwa ujumla. Muhula wa wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021. Hivyo unatakiwa kufika shuleni mapema na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021

"Medical examination form" ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospitali ya serikali imeambatanishwa, kadhalika fomu hii ukishaikamilisha utaikabidhi kwa makamu mkuu wa shule mara tu utakaporipoti.

#### **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

##### **1: SARE ZA SHULE**

###### **(a) WAVULANA**

- ❖ Suruali rangi danu ya mzee iliyoshonwa kwa malinda matatu kila upande na isiyobana au kwa maelezo zaidi unapaswa kuonana na uongozi wa shule
- ❖ Shati nyeupe mikono mifupi mbili (2) za tetroni
- ❖ Soksi nyeusi jozi mbili (2)
- ❖ Viatu vya ngozi nyeusi (siyo buti) jozi mbili (2) vya kamba
- ❖ Raba jozi moja, soksi ndefu, bukta rangi ya bluu kwa ajili ya michezo.
- ❖ Counter books (daftari kubwa) tisa kuanzia quire 2 kwa matumizi yako katika masomo

- ❖ Mkebe ( mathematical set)

(b) WASICHANA

- ❖ Sketi rangi damu ya mzee rinda boksi ndefu inayovuka magoti au unapaswa kuonana na uongozi wa shule kwa maelezo zaidi.
- ❖ Shati nyeupe mikono mifupi mbili (2) za tetroni
- ❖ Soksi nyeupe jozi mbili (2)
- ❖ Viatu ngozi nyeusi jozi mbili (2) visivyo na visigino virefu
- ❖ Raba jozi moja, soksi ndefu, track suit rangi ya bluu kwa ajili ya michezo
- ❖ Kwa watakaoshona ijabu, ziwe ndefu zinazofunika mikono
- ❖ Counter books (daftari kubwa) tisa (9) kuanzia quire 2 kwa matumizi yako katika masomo
- ❖ Mkebe (mathematical set)

## **2: SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

2.1 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu namba 25 ya mwaka 1978.

Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo muhimu ya msingi yafuatayo

- a. Kutumia lugha ya kiingereza kama nyenzo kuu ya mawasiliano uwapo shuleni
- b. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- c. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu
- d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo kwa wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f. Kutunza usafi wa mwili na mazingira yote ya shule
- g. kuvaa sare za shule wakati wote
- h. Huruhusiwi kwenda kwenye kumbi za starehe. Mfano baa, kumbi za muziki (disco), vigodoro n.k

2.2 ***Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ufukuzwe shule***

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji sigara, bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau bendera na wimbo wa taifa
8. Kuoia au kuolewa
9. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule au kusababisha mimba
10. Kutoa mimba
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi

***KARIBU NAMWAWALA SEKONDARI***

.....  
MKUU WA SHULE